

Auckland Regional Public Health Service
Rātonga Hauora ā Iwi o Tamaki Makaurau



Working with the people of Auckland, Counties Manukau and Waitemata

**Wakati daktari wako
anapokuelekeza kwa
mtaalamu katika
hospitali au zahanati**

Doctor Referral—Swahili
June 2011

Auckland Regional Public Health Service
Rātonga Hauora ā Iwi o Tamaki Makaurau



Working with the people of Auckland, Counties Manukau and Waitemata

Daktari amekuelekeza kwa mtaalamu katika hospitali au zahanati. Ni bure na hautagharamika pesa zozote.

Utapata barua kutoka kwa hospitali au zahanati pamoja na saa za siku na wakati wa kumuona daktari. Kwa kawaida inachukua miezi mitatu kupewa siku na wakati wa kumuona daktari.

Hakikisha kuwa umeisoma barua wakati unapoipokea au muulize mtu akusomee barua. Lazima ufuata maelezo ili kuhakikisha kuwa utaenda siku na wakati wa kumuona daktari.

Kama unahitajika waweza kuuliza hospitali au zahanati wakupe mkalimani. Waweza kuomba wa kiume au wa kike pamoja na lahaja haswa ya lugha yako.

Kama unahitaji kubadili au kupangua siku na wakati wa kumuona daktari lazima upigie simu hospitali au zahanati.

Kama ukikosa kwenda siku na wakati wa kumuona daktari yaweza kuchukua muda mrefu kupata siku na wakati wa kumuona daktari nyingine mpya na waweza kutolewa kwenye orodha ya wanaogojea.

Hospitali itamtumia ripoti daktari (GP) wako. Kama unaye daktari (GP) zaidi ya mmoja ripoti itaenda kwa daktari aliyekuelekeza kwa hospitali au zahanati.

Utahitaji kujipanga Kufika hospitalini au kwenye zahanati kwa ajili ya kumuona daktari.

Utahitaji kupata usafiri unaokufikisha kwenye hospitali au zahanati katika wakati maridhawa kabla ya wakati wa kumuona daktari wako. Ruhusu nusu saa kwa kutafuta zahanati kama hujawahi kufika pale tena. Ni muhimu kuwahi saa ili usikose nafasi yako..

Kama una watoto itasaidia kama una jamaa au rafiki ambaye atawatunza pale nyumbani au pale unapofika hospitalini. Hii ni jukumu yako kupangia.